TANGAZO LA SERIKALI NA. 809 la tarehe 13/9/2024

SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE,
NA.13 YA 2023

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 35)*

KANUNI ZA BIMA YA AFYA KWA WOTE ZA MWAKA 2024

*Jina Kanuni*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
USAJILI WA SKIMU ZA BIMA YA AFYA

3. Maombi na vigezo vya usajili.
4. Maamuzi kuhusu maombi ya usajili.
5. Usajili na cheti cha usajili.
6. Kukataa usajili.
7. Kuhuisha usajili.
8. usajili wa skimu zilizoruhusiwa kuendelea kutoa huduma.
9. Utaratibu kabla ya kufutwa kwa skimu ya bima ya afya.
10. Kuomba kufutiwa usajili.
11. Taarifa ya kufutwa kwa usajili wa skimu ya bima ya afya.
12. Rejesta ya skimu za bima za afya.

SEHEMU YA TATU
UTAMBUZI NA USAJILI WA WATU WASIO NA UWEZO

13. Majukumu ya mamlaka ya utambuzi.

14. Kanzidata ya watu wasio na uwezo.
15. Usimamizi wa Mfuko.
16. Ugharamiaji wa huduma za afya kwa watu wasio na uwezo.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI NA UDHIBITI WA HUDUMA ZA BIMA YA AFYA

17. Usimamizi na udhibiti wa huduma za bima ya afya.
18. Kanzidata ya vituo vya kutolea huduma za afya.
19. Ukaguzi wa skimu za bima ya afya.

SEHEMU YA TANO
USAJILI WA WANACHAMA KATIKA SKIMU ZA BIMA YA AFYA

20. Usajili wa wanachama katika skimu za bima ya afya.
21. Miongozo ya usajili wa wanachama.
22. Muda wa kusubiri kuanza kupata huduma.
23. Usajili wa waajiriwa katika skimu ya bima ya afya.
24. Ukomo wa uanachama.
25. Ukomo wa mtegemezi.
26. Usitishaji wa skimu ya bima ya afya kutoa huduma.
27. Notisi ya kituo kusitisha kutoa huduma za afya
28. Uwasilishaji wa malalamiko dhidi ya kusudio la kituo kusitisha utoaji huduma.
29. Uamuzi wa Mamlaka kuhusu kusudio la kituo kusitisha utoaji huduma.

SEHEMU YA SITA
VITITA VYA MAFAO

30. Muda wa kunufaika na kitita cha mafao ya huduma muhimu.
31. Viwango vya uchangiaji kwa kitita cha mafao ya huduma muhimu.
32. Maboresho ya kitita cha mafao ya huduma muhimu.
33. Uzingatiaji wa taratibu za rufaa.
34. Miongozo ya utoaji wa kitita cha mafao ya huduma muhimu.
35. Kitita cha huduma za ziada.

SEHEMU YA SABA
UTARATIBU WA MALIPO KWA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

36. Uwasilishaji wa madai.

37. Ulipaji wa madai.
38. Uchunguzi na usuluhishi wa madai.
39. Ushughulikiaji wa malalamiko.
40. Usuluhishi na utatuzi wa Migogoro.
41. Rufaa dhidi ya maamuzi ya Mamlaka.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA JUMLA

42. Matumizi ya Kanuni za Bima.
43. Utaratibu wa uwekaji wa amana.
44. Utaratibu wa kuhama skimu.
45. Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya michango.
46. Makosa na adhabu dhidi ya skimu za bima ya afya.
47. Hatua ambazo Mamlaka inaweza kuchukua dhidi ya skimu ya bima ya afya.
48. Kufuta.

SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE,
NA.13 YA 2023

KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 35)*

KANUNI ZA BIMA YA AFYA KWA WOTE ZA MWAKA 2024

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitaitwa Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote za Mwaka 2024.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 394

"Baraza la Rufaa la Bima" maana yake Baraza la Rufaa la Bima lililoanzishwa chini ya kifungu cha 126 cha Sheria ya Bima;

Na. 13 ya 2023

"Sheria" maana yake Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote;

"rejesta" maana yake rejesta inayotunzwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria, ambamo kutahifadhiwa taarifa za skimu za bima za afya au wanachama wake waliosajiliwa na walio katika mfumo wa maandishi au kieletroniki;

"Mamlaka" maana yake Mamlaka ya Usimamizi wa Bima iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bima;

Sura ya 351

"mamlaka za utambuzi wa watu wasio na uwezo" maana yake ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Takwimu, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), na inajumuisha mamlaka nyingine yoyote yenye dhamana Nchini ya kusimamia programu inayohusika na utambuzi wa watu wasio na uwezo;

Sura ya 394

"Msuluhishi" maana yake Msuluhishi wa Migogoro ya Bima anayerejelewa chini ya Sehemu ya Tisa ya Sheria ya Bima; na

"Mfuko" maana yake mfuko wa kugharamia watu wasio na uwezo ulioanzishwa chini ya Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## USAJILI WA SKIMU ZA BIMA YA AFYA

Maombi na vigezo vya usajili

3.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kutoa huduma za bima ya afya kama skimu ya bima ya afya binafsi atawasilisha kwa Mamlaka maombi ya usajili katika Fomu Na. I iliyobainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

(2) Maombi chini ya kanuni ndogo ya (1) yataambatishwa na-

(a) nakala ya cheti cha usajili wa kampuni;
(b) uthibitisho wa maazimio ya bodi ya wakurugenzi ya kampuni ya kuanzisha skimu ya bima ya afya;
(c) tathmini ya awali ya mpango wa uendeshaji wa skimu ya bima ya afya;
(d) taarifa kuhusu maeneo ya kijiografia ambayo kampuni inakusudia kutoa huduma za bima ya afya;
(e) taarifa binafsi za mtendaji mkuu wa kampuni;
(f) uthibitisho wa malipo ya kodi kwa Serikali;

T.S Na. 372 la 2009

(g) uthibitisho wa mtaji wa skimu ya bima ya afya kwa mujibu wa Kanuni za Bima za Mwaka 2009;
(h) uthibitisho wa sifa za wakurugenzi na menejimenti ya kampuni kama zitakavyobainishwa kwenye miongozo itakayotolewa na Mamlaka;
(i) uthibitisho wa malipo ya ada ya usajili na ada ya mwaka inayotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 158 cha Sheria ya Bima; na
(j) taarifa nyingine muhimu kwaajili ya usajili ambayo Mamlaka inaweza kuhitaji.

Maamuzi kuhusu maombi ya usajili

4.-(1) Mamlaka itapaswa, kwa maombi ya usajili yaliyotimiza vigezo vya maombi, kufanyia kazi maombi ya usajili na kutoa maamuzi, ndani ya siku thelathini tangu kupokea maombi hayo.

(2) Endapo Mamlaka imepokea maombi ambayo hayajatimiza vigezo vya maombi, inaweza, kabla ya kutoa uamuzi kuhusu maombi hayo, kumtaka mwombaji, ndani ya kipindi kisichozidi siku thelathini-

(a) kuwasilisha nyaraka au taarifa zilizokosekana; au

(b) kurekebisha makosa hayo ili kukidhi vigezo vya usajili.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), endapo Mamlaka itahitaji kufanya uchunguzi zaidi wa maombi yaliyowasilishwa, inaweza kufanya hivyo ndani ya siku tisini tangu tarehe ya kupokea maombi.

(4) Mamlaka itakuwa na wajibu wa kumjulisha kwa maandishi mwombaji kuhusu muda wa nyongeza wa uchunguzi.

Usajili na cheti cha usajili

5.-(1) Mamlaka, baada ya kujiridhisha kuwa muombaji amekidhi vigezo vyote vya usajili, itasajili skimu ya bima ya afya na kutoa cheti cha usajili.

T.S Na. 372 la 2009

(2) Cheti cha usajili kitakachotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) kitakuwa kama kilivyoainishwa kwenye Kanuni za Bima za Mwaka 2009.

(3) Cheti cha usajili kilichotolewa chini ya Kanuni hizi kitakuwa halali kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kutolewa kwake.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (3), Mamlaka inaweza kutoa cheti cha usajili kwa skimu ya bima ya afya kwa kipindi kisichozidi miaka mitano kwa kuzingatia tathmini ya uendelevu wa skimu husika.

(5) Endapo Mamlaka itabaini kuwa skimu ya bima ya afya inashindwa kuwa na uhimilivu kulingana na uhai wa cheti cha usajili, inaweza kupunguza muda wa uhai wa cheti cha usajili kukidhi kipindi cha uhimilivu.

Kukataa usajili

6.-(1) Mamlaka inaweza kukataa maombi ya usajili wa skimu ya bima ya afya iwapo muombaji-

(a) ameshindwa kukidhi vigezo vya usajili chini ya kanuni hizi; au

(b) ameshindwa kutimiza vigezo chini ya kanuni ya 4(2).

(2) Endapo Mamlaka itakataa kusajili skimu ya bima ya afya, itamjulisha mwombaji kwa maandishi sababu za uamuzi kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 4.

Kuhuisha usajili

7.-(1) Skimu ya bima ya afya, ndani ya kipindi cha siku thelathini kabla ya cheti cha usajili kufikia ukomo, itawasilisha maombi ya kuhuisha usajili:

Isipokuwa kwamba-

(a) kwa kadri itakavyohitajika, skimu ya bima ya afya inaweza kupatiwa cheti kipya baada ya Mamlaka kuhuisha usajili; na

(b) skimu ya bima ya afya haitakuwa na wajibu wa kuomba upya usajili kwa mujibu wa kanuni ya 3.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), skimu ya bima ya afya yenye cheti cha usajili cha ukomo wa zaidi ya mwaka mmoja itatakiwa kuwasilisha maombi ya kuhuisha usajili kila mwaka.

(3) Skimu ya bima ya afya inayokusudia kuomba kuhuisha usajili itawasilisha maombi kwa Mamlaka kupitia Fomu Na. 2 iliyobainishwa kwenye Jedwali la Kanuni hizi.

(4) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza kuongeza muda wa kuhuisha usajili kwa kuzingatia miongozo itakayoitoa.

(5) Mamlaka inaweza kukataa maombi ya kuhuisha usajili endapo-

(a) skimu ya bima ya afya inatakiwa kufutiwa usajili kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi; au

T.S Na. 372 la 2009

(b) skimu ya bima ya afya haijakidhi vigezo kuhusu uhitaji wa mtaji kwa mujibu wa Kanuni za Bima za mwaka 2009.

(6) Skimu ya bima ya afya itakayokidhi vigezo kwa mujibu wa kanuni hii itatakiwa kulipa ada ya mwaka.

usajili wa skimu zilizoruhusiwa kuendelea kutoa

8.-(1) Mamlaka itazitaka skimu ya bima ya afya ya umma na binafsi zinazotambulika hivyo kwa mujibu

huduma

wa kifungu cha 8 na 9(2) cha Sheria, kuwasilisha taarifa mbalimbali zilizorejewa katika kanuni ya 3(2) kwa madhumuni ya kutolewa kwa cheti cha usajili na hifadhi ya kumbukumbu za usajili.

(2) Skimu za bima ya afya zilizorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) zitaendelea kuwahudumia wanachama na wanufaika kwa kuzingatia mikataba ya awali hadi itakapofikia ukomo wake, na baada ya hapo utaratibu wa usajili wa wanachama chini ya Kanuni hizi utazingatiwa.

(3) Isipokuwa kwa masharti ya kanuni ya 4, 5 na 6 ya Kanuni hizi, skimu zilizoruhusiwa kuendelea kutoa huduma zinapaswa kuzingatia masharti mengine ya usajili ikiwemo masharti kuhusu ulipaji wa ada ya usajili na ada ya mwaka.

Utaratibu kabla ya kufutwa kwa skimu ya bima ya afya

9.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 12 cha Sheria, notisi ya kusudio la kufuta skimu ya bima ya afya itathibitika kuwa imepokelewa na skimu ya bima ya afya iwapo imewasilishwa kupitia anuani ya makazi ya kampuni au taasisi iliyotolewa wakati wa usajili wa skimu ya bima ya afya.

(2) Skimu ya bima ya afya isiyoridhishwa na kusudio la kufutiwa usajili inaweza, ndani ya siku tisini za notisi, kutoa uwakilishi wake wa maandishi kwa Mamlaka, na Mamlaka itatoa maamuzi ya uwakilishi huo kabla ya kufuta usajili.

(3) Katika kulinda maslahi ya wanachama wa skimu ya bima ya afya inayokusudiwa kufutiwa usajili, Mamlaka inaweza kuchukua hatua yoyote kama ilivyoainishwa katika kanuni ya 47 kabla ya kufuta usajili, na skimu ya bima ya afya itakuwa na wajibu wa kuzingatia amri au maelekezo yatokanayo na hatua ya Mamlaka.

Kuomba kufutiwa usajili

10.-(1) Pale ambapo skimu ya bima ya afya inakusudia kuomba kufutiwa usajili, itatoa kwa Mamlaka notisi ya siku tisini ya kusudio kabla ya tarehe ya kusitisha huduma za bima ya afya, ikibainisha sababu za kutaka kufutiwa usajili.

(2) Kabla ya kufuta usajili chini ya kanuni ndogo (1), Mamlaka itaitaka skimu ya bima ya afya kuwasilisha taarifa zifuatazo-

(a) taarifa ya namna wanachama watakavyohudumiwa mpaka muda wa uanachama wao utakapokoma;
(b) taarifa za madai ya vituo vilivyoingia mikataba na skimu ya bima ya afya na namna yatakavyolipwa; na
(c) tathmini ya uhai wa skimu ya bima ya afya.

(3) Mamlaka ndani ya kipindi cha siku tisini, baada ya kufanya uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa na skimu ya bima ya afya inaweza kukubali au kukataa ombi hilo na kuainisha masharti ya kutekeleza kulingana na miongozo ya Mamlaka.

Taarifa ya kufutwa kwa usajili wa skimu ya bima ya afya

11. Mamlaka ndani ya siku saba tangu tarehe ya kufuta usajili wa skimu ya bima ya afya, na kwa kupitia vyombo vya habari vinavyofikia wananchi wengi, itautaarifu umma kuhusu kufutwa kwa skimu na kuwataarifu wanachama na vituo viliyoingia mkataba na skimu hiyo kuhusu namna ambavyo wanachama na wanufaika wa skimu iliyofutwa watakavyopata huduma.

Rejesta ya skimu za bima za afya

12.-(1) Mamlaka itaweka na kutunza rejesta ya skimu za bima za afya kwa namna iliyobainishwa katika Fomu Na. 3 ya Jedwali la Kanuni hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), rejesta inayotajwa katika kanuni ndogo ya (1) itakuwa na taarifa zifuatazo-

(a) jina, anuani na mawasiliano ya skimu ya bima ya afya;
(b) namba ya usajili;
(c) tarehe ya usajili;
(d) idadi ya wanachama na wanufaika waliosajiliwa na skimu ya bima ya afya;
(e) taarifa ya waajiri walioingia mkataba na skimu ya bima ya afya;
(f) taarifa ya vituo vilivyoingia mkataba na skimu ya bima ya afya; na

(g) taarifa yoyote ambayo Mamlaka itaona inafaa.

(3) Rejesta ya skimu ya bima ya afya itatakiwa kusasishwa kila mwaka.

## SEHEMU YA TATU
## UTAMBUZI NA USAJILI WA WATU WASIO NA UWEZO

Majukumu ya mamlaka ya utambuzi

13.-(1) Kwa madhumuni ya fedha za Mfuko kuanza kutumika kugharamia watu wasio na uwezo, Wizara itaziomba mamlaka za utambuzi wa watu wasio na uwezo kuandaa na kuwasilisha kwake, katika muda utakaobainishwa na Wizara, orodha ya watu wasio na uwezo.

(2) Mara baada ya kupokea maombi ya Wizara, mamlaka za utambuzi zitaandaa orodha ya watu wasio na uwezo na kuwasilisha Wizarani katika muda uliopangwa.

(3) Kwa kuzingatia wigo mpana wa uwakilishi wa makundi mbalimbali katika jamii ikiwemo makundi yenye mahitaji maalum na kwa kuzingatia muda uliopangwa na utaratibu uliokubalika baina ya Wizara na mamlaka za utamhuzi, mamlaka hizo za utambuzi zitashirikisha wadau kwa ajili ya uhakiki wa orodha ya watu wasio na uwezo iliyoandaliwa.

(4) Mamlaka za utambuzi zitatunza kumbukumbu ya orodha ya watu wasio na uwezo na kuwasilisha kwa Waziri kwa kadri itakavyokuwa ikihitajika.

Kanzidata ya watu wasio na uwezo

14.-(1) Wizara itatunza kanzidata ya watu wasio na uwezo ambao wanakidhi kugharamiwa bima za afya kupitia Mfuko.

(2) Kila baada ya miaka mitatu, mamlaka za utambuzi zitafanya tathmini na kuishauri Wizara kuhusu watu wanaopaswa kuondolewa au kujumuishwa katika kanzidata.

Usimamizi wa Mfuko

15.-(1) Mfuko wa kugharamia bima za afya kwa watu wasio na uwezo utasimamiwa na kuratibiwa na Wizara.

(2) Katika kuratibu na kusimamia Mfuko, Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo-

(a) kufuatilia upatikanaji wa fedha za Mfuko;
(b) kufuatilia upatikanaji wa wanufaika wa Mfuko;
(c) kuratibu usajili wa wanufaika wa Mfuko;
(d) kutunza kumbukumbu za wanufaika wa Mfuko;
(e) kushauri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Mfuko; na
(f) kutekeleza majukumu mengine yoyote kadri itakavyoelekezwa.

(3) Uendeshaji wa kila siku wa Mfuko utasimamiwa na skimu ya bima ya afya umma.

Ugharamiaji wa huduma za afya kwa watu wasio na uwezo

16.-(1) Watu waliotambuliwa na kuingizwa katika kanzidata ya watu wasio na uwezo watapata huduma za afya kwa utaratibu wa bima ya afya chini ya skimu ya bima ya afya ya umma kwa kugharamiwa na Serikali kupitia Mfuko.

(2) Wizara itawasilisha katika skimu ya bima ya afya ya umma orodha ya watu wasio na uwezo na michango yao kwa ajili ya kugharamiwa bima ya afya.

(3) Skimu ya bima ya afya ya umma, baada ya kupokea orodha na michango ya watu wasio na uwezo itawasajili na kutoa utambulisho ili kuwawezesha watu hao kupata huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma au vituo vya kutolea huduma za afya vya binafsi vilivyoingia mkataba na Serikali.

(4) Watu wasio na uwezo waliosajiliwa watakuwa na haki ya kupata huduma za afya kulingana na kitita cha mafao walichogharamiwa kupitia Mfuko.

(5) Endapo watu wasio na uwezo watahitaji huduma za ziada nje ya kitita cha mafao walichogharamiwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (4), wanaweza kupata huduma hizo kupitia Mfuko kwa kuzingatia utaratibu wa rufaa.

(6) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (5), Wizara itaandaa mwongozo wa rufaa kwa huduma za ziada nje ya kitita cha mafao walichogharamiwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (4).

(7) Waziri, kupitia tangazo la kawaida katika

gazeti la serikali, atautangaza kwa umma, muongozo wa rufaa unaorejewa katika kanuni ndogo ya (6).

## SEHEMU YA NNE
## USIMAMIZI NA UDHIBITI WA HUDUMA ZA BIMA YA AFYA

Usimamizi na udhibiti wa huduma za bima ya afya

17.-(1) Mamlaka itasimamia na kudhibiti skimu za bima ya afya kwa kuhakikisha zinatoa huduma za bima ya afya kwa wanachama wake na vituo vya huduma ya afya vilivyoingia mkataba na skimu kwa kuzingatia yafuatayo-

(a) kutoendesha skimu ya bima ya afya bila ya cheti halali cha usajili;
(b) wanachama na wanufaika wa skimu ya bima ya afya wanapatiwa huduma bila ya usumbufu wala ubaguzi;
(c) mtu anayestahili kujiandikisha katika skimu ya bima ya afya anasajiliwa bila ya vikwazo vyovyote ili mradi ametimiza masharti ya usajili;
(d) kutokuwepo kwa vigezo vya usajili kwa wanachama visivyotekelezeka;
(e) utoaji wa huduma kwa kuzingatia mpango wa utoaji huduma wa skimu ya bima ya afya ulioidhinishwa na Mamlaka; na
(f) ushughulikiaji kwa wakati wa malalamiko kuhusu bima ya afya.

Kanzidata ya vituo vya kutolea huduma za afya

18.-(1) Mamlaka itatunza kanzidata ya vituo vya huduma za afya vilivyoingia mkataba na skimu za bima ya afya ikijumuisha taarifa zifuatazo:

(a) jina na anuani ya kituo cha huduma za afya;
(b) ngazi ya kituo cha kutolea huduma za afya;
(c) umiliki wa kituo cha huduma za afya;
(d) namba ya usajili wa kituo cha kutolea huduma za afya;
(e) tarehe ya usajili wa kituo cha huduma za afya;
(f) tarehe ya kuingia mkataba na skimu ya bima ya afya;
(g) muda wa mkataba kati ya kituo cha kutolea

huduma za afya na skimu ya bima ya afya;

(h) jina la skimu iliyoingia mkataba na kituo; na

(i) tarifa nyingine yoyote ambayo Mamlaka itaona inafaa.

(2) Mamlaka itakuwa na wajibu wa kusasisha kanzidata mara kwa mara kwa kadiri mabadiliko yatakavyojitokeza.

(3) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo (1), skimu ya bima ya afya itatakiwa-

(a) kuwasilisha kwa Mamlaka kwa namna itakayobainishwa katika muongozo uliowekwa na Mamlaka; na

(b) kutunza na kuweka kwenye tovuti yake,

kanzidata ya vituo vya kutolea huduma vilivyoingia mkataba na skimu husika.

Ukaguzi wa skimu za bima ya afya

19.-(1) Mamlaka itafanya ukaguzi wa skimu za bima ya afya kila mwaka kwa kuzingatia taratibu na miongozo ya ukaguzi iliyowekwa na Mamlaka.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza kufanya ukaguzi maalum wakati wowote itakapoona inafaa.

(3) Katika kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka itapaswa kutoa notisi ya siku tatu kwa skimu ya bima ya afya kabla ya ukaguzi kufanyika.

## SEHEMU YA TANO
## USAJILI WA WANACHAMA KATIKA SKIMU ZA BIMA YA AFYA

Usajili wa wanachama katika skimu za bima ya afya

20.-(1) Kila raia au mkazi katika sekta rasmi na isiyo rasmi atakuwa na haki ya kusajiliwa katika skimu ya bima ya afya kwa utaratibu utakaowekwa na skimu ya bima ya afya kupitia miongozo yake ambayo itaidhinishwa na Mamlaka.

(2) Skimu ya bima ya afya itahakikisha mifumo ya usajili inayotumika inamuwezesha mwanachama kupata utambulisho ndani ya siku saba tangu tarehe ya kukamilika kwa usajili.

(3) Skimu ya bima ya afya itatakiwa kuhakikisha

huduma za usajili zinapatikana hadi ngazi ya kijiji na mtaa.

(4) Skimu ya bima ya afya itahakikisha inatunza kanzidata ya wanachama waliosajiliwa kulingana na miongozo iliyowekwa na Mamlaka.

(5) Skimu ya bima ya afya itatakiwa kutoa notisi ya ukomo wa uanachama kwa mwanachama angalau siku thelathini kabla ya tarehe ya kufikia ukomo wa uanachama.

(6) Mwanachama anayechangia kwa utaratibu wa mkupuo kwa mwaka atachukuliwa kuwa amehuisha uanachama wake iwapo atalipia katika skimu ya bima ya afya kiwango cha uchangiaji ndani ya siku thelathini baada ya tarehe ya kufikia ukomo wa uanachama.

(7) Mwanachama atakayeshindwa kuhuisha uanachama wake kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (6) atapaswa kujisajili upya kwa kuzingatia utaratibu uliobainishwa katika Kanuni hizi.

Miongozo ya usajili wa wanachama

21.-(1) Bila kuathiri kanuni ya 20(1), na kwa kuzingatia miongozo iliyowekwa na Mamlaka, skimu ya bima ya afya itatakiwa kuwasilisha kwa Mamlaka miongozo yake ya usajili wa wanachama kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya kuanza kutumika kwa miongozo hiyo.

Mamlaka, katika kuidhinisha miongozo ya usajili wa wanachama itakayowasilishwa kwake na skimu za bima ya afya, itazingatia masuala yafuatayo-

(a) nyaraka mbalimbali kwa ajili ya utambuzi na uhakiki wa wanachama;
(b) utaratibu wa utambulisho wa wanachama na wanufaika;
(c) utaratibu wa usitishaji na urejeshwaji wa huduma kwa wanachama na wanufaika;
(d) uhitaji wa kumbukumbu za uanachama wa awali katika skimu ya bima ya afya nyinginezo, kama zipo; na
(e) taarifa nyingine muhimu kwa kadri itakavyoelekezwa na Mamlaka.

Muda wa kusubiri kuanza kupata huduma

22.-(1) Skimu ya bima ya afya inaweza kuweka muda wa kusubiri wa mwanachama na mnufaika aliyesajiliwa katika skimu hiyo kabla ya kuanza kunufaika na huduma za bima ya afya

Isipokuwa kwamba, muda huo wa kusubiri hautazidi siku thelathini tangu tarehe ya mwanachama au mnufaika kusajiliwa.

(2) Masharti ya kanuni ndogo ya (1) hayatawahusu-

(a) waajiriwa katika sekta ya umma na sekta rasmi binafsi;
(b) watu wasio na uwezo wanaogharamiwa na Serikali;
(c) watu wote waliokuwa wanachama hai wa skimu ya umma wakati wa kuanza kutumika kwa Sheria; au
(d) wanachama ambao ni wanafunzi wanaojiunga kwa makundi.

(3) Katika uwekaji wa muda wa kusubiri, skimu ya bima ya afya itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa muda huo hauathiri uhai na uendelevu wa skimu ya bima ya afya.

(4) Kila skimu ya bima ya afya katika miongozo yake ya usajili wa wanachama, itabainisha muda wa kusubiri.

Usajili wa waajiriwa katika skimu ya bima ya afya

23.-(1) Mwajiri katika sekta rasmi binafsi ataingia mkataba na skimu ya bima ya afya moja kwa lengo la kuwasajili waajiriwa wake ili kupata kitita cha mafao cha huduma muhimu au kitita cha huduma za ziada:

Isipokuwa kwamba, mwajiri anaweza kuingia mkataba na skimu ya bima ya afya nyingine kwa lengo la kuwawezesha waajiriwa wake kupata huduma za kitita cha ziada.

(2) Skimu ya bima ya afya ya umma inaweza kuingia mkataba na mwajiri katika sekta ya umma au binafsi kwa masharti yatakayowekwa kwa mujibu wa Sheria inayosimamia skimu ya bima ya afya ya umma.

(3) Katika kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (1), mwajiri katika sekta rasmi binafsi atawashirikisha

waajiriwa katika kuchagua skimu ya bima ya afya wanayopaswa kuingia nayo mkataba.

(5) Mwajiri ambaye atamsajili mwajiriwa katika skimu ya bima ya afya atawasilisha mchango wa mwajiriwa kwa skimu ya bima ya afya kabla au ifikapo tarehe kumi na tano ya mwezi unaofuata tangu tarehe ya kumsajili mwajiriwa.

Ukomo wa uanachama

24.-(1) Kwa madhumuni ya kifungu cha 28(1) cha Sheria, uanachama utakomo endapo-

(a) mwanachama ambaye ni mwajiriwa katika sekta ya umma au sekta rasmi binafsi ataacha kuchangia kwa kipindi cha miezi mitatu mfululizo; na
(b) mwanachama ambaye anachangia kwa mwaka ataacha kuchangia mwezi mmoja baada ya mwaka wa uchangiaji kupita.

(2) Endapo mwanachama anayechangia kupitia makato ya mshahara atafikia ukomo wa uanachama, wategemezi wake wataendelea kunufaika kwa kipindi cha mwezi mmoja tangu kupokea mchango wa mwisho.

Ukomo wa mtegemezi

25. Kwa kuzingatia kifungu cha 3 cha Sheria, endapo mtegemezi ambaye ni-

(a) mtoto wa mwanachama wa kuzaa, kuasili au wa kambo; au
(b) ndugu wa damu wa mwanachama,

atafikisha umri wa miaka ishirini na moja, mtegemezi huyo atakuwa amefikia ukomo wa utegemezi.

Usitishaji wa skimu ya bima ya afya kutoa huduma

26. Skimu ya bima ya afya inaweza kusitisha utoaji wa huduma kwa mwanachama au mnufaika endapo-

(a) mwanachama ambaye ni mwajiriwa katika sekta ya umma au sekta rasmi binafsi ataacha kuchangia kwa kipindi cha mwezi mmoja; au
(b) mwanachama ambaye anachangia kwa mwaka ataacha kuchangia baada ya mwaka wa kuchangia kuisha.

Notisi ya kituo kusitisha kutoa huduma za afya

27.-(1) Kituo cha kutolea huduma za afya kinacho kusudia kusitisha utoaji wa huduma za afya kwa wanachama na wanufaika wa skimu ya bima ya afya kitatoa notisi ya maandishi ya siku tisini kwa skimu na nakala kwa Mamlaka ikibainisha kusudio la kusitisha huduma na sababu za kusudio hilo.

(2) Katika kipindi cha notisi, kituo cha kutolea huduma za afya kitatakiwa-

(a) kuweka utaratibu wa namna ya kukamilisha au uhamisho wa utoaji wa huduma kwa wanufaika wa skimu ya bima ya afya na nakala ya taarifa hiyo kuwasilishwa kwa Mamlaka; na

(b) kupokea na kutekeleza maelekezo ya Mamlaka kuhusiana na taarifa iliyowasilishwa kwake chini ya aya (a) au uamuzi wowote uliotokana na malamiko yaliyowasilishwa kwa Mamlaka.

Uwasilishaji wa malalamiko dhidi ya kusudio la kituo kusitisha utoaji huduma

28.-(1) Kwa madhumuni ya kanuni ya 27(2)(b), skimu ya bima ya afya itakapopokea taarifa ya kusudio la usitishwaji wa huduma kwa wanachama wake, itatoa tangazo la umma kwa namna itakayoweza kuwafikia wananchi walio wengi kwa lengo la kutoa fursa kwa mtu kutoa pingamizi kwa Mamlaka.

(2) Mtu yeyote ambaye ataathirika na usitishwaji wa utoaji wa huduma anaweza kuwasilisha malalamiko yake kwa Mamlaka ndani ya kipindi kisichozidi siku ishirini na moja tangu tarehe ya tangazo la umma kutolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1).

Uamuzi wa Mamlaka kuhusu kusudio la kituo kusitisha utoaji huduma

29. Mamlaka ndani ya kipindi cha siku thelathini, baada ya kupokea malalamiko, itatoa uamuzi ufuataao-

(a) endapo usitishwaji wa utoaji huduma za afya utaathiri unufaikaji wa huduma au mkataba baina yake na skimu ya bima ya afya, kituo hicho kitakuwa na wajibu wa kufidia hasara kwa mnufaika au skimu ya bima ya afya kwa kuzingatia makubaliano yaliyopo baina yake na skimu; au

(b) endapo hakuna pingamizi lolote kutoka kwa mtu, skimu ya bima ya afya au Mamlaka, kituo cha kutolea huduma kitasitisha utoaji wa huduma na kuitaarifu skimu ya bima ya afya na nakala kwa Mamlaka.

.

## SEHEMU YA SITA
## VITITA VYA MAFAO
### *(a) Kititia Cha Mafao ya Huduma Muhimu*

Muda wa kunufaika na kitita cha mafao ya huduma muhimu

30.-(1) Mwanachama na mnufaika wa skimu za bima ya afya watakuwa na haki ya kupata huduma za kitita cha mafao ya huduma muhimu kama kilivyobainishwa katika Sehemu A ya Jedwali la Sheria, iwapo ni mwanachama-

(a) anayechangia kwa utaratibu wa kulipa kwa mkupuo mmoja kwa mwaka, kwa kipindi cha mwaka mmoja tangu tarehe ya kusajiliwa au baada ya muda wa kusubiri kuisha; na

(b) ambaye ni mwajiriwa katika sekta ya umma na sekta rasmi binafsi, kwa kipindi chote cha uanachama wake.

(2) Dawa zitakazotolewa kwa wanufaika wa skimu za bima ya afya kwa kitita cha mafao ya huduma muhimu zitaandikwa kwa majina ya asilia na kwa kuzingatia Orodha ya Taifa ya Dawa Muhimu inayotolewa na Wizara.

Viwango vya uchangiaji kwa kitita cha mafao ya huduma muhimu

31.-(1) Kila mwajiri chini ya sekta ya umma na sekta rasmi binafsi aliyejisajili katika skimu ya bima ya afya ya umma atawasilisha katika skimu hiyo kiwango cha uchangiaji kwa mujibu wa sheria ya bima ya afya ya umma, ambapo ndani yake mwajiri atachangia nusu au zaidi ya kiwango hicho, na kiwango kilichosalia kitachangiwa na mwajiriwa:

Isipokuwa kwamba, mwajiri anaweza kuchangia kiwango chote cha uchangiaji.

(2) Waziri atatoa tangazo la umma kwa namna itakayoweza kuwafikia wananchi walio wengi viwango vya uchangiaji pamoja na huduma zitakazopatikana

katika kitita cha mafao ya huduma muhimu kwa-

(a) mwanachama kutoka sekta isiyo rasmi atakayejisajili katika skimu ya bima ya afya ya umma;

(b) mwanachama ambaye anachangia kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) na (2)(a) na anahitaji kusajili mtegemezi mwingine anayeruhusiwa kwa mujibu wa Sheria;

(c) mwanachama ambaye ni mwanafunzi anayejiunga kwa makundi.

(3) Endapo mwanachama ana mwenza zaidi ya mmoja, mwenza huyo anaweza kusajiliwa kama mwanachama na anaweza kusajili wategemezi wanaoruhusiwa kwa mujibu wa Sheria.

(4) Waziri atatoa tangazo la umma kwa namna itakayoweza kuwafikia wananchi walio wengi litakaloainisha aina za Kitita cha Mafao ya Huduma Muhimu ambavyo vitatolewa na Skimu ya Bima ya Afya ya Umma baada ya kuthibitishwa na Mamlaka.

Maboresho ya kitita cha mafao ya huduma muhimu

32.-(1) Kwa madhumuni ya kuhakikisha huduma za kitita cha mafao ya huduma muhimu zinaendana na mahitaji ya huduma za afya kwa wakati husika, Waziri baada ya kushauriwa na Mamlaka anaweza kufanya maboresho ya kitita cha mafao ya huduma muhimu kwa-

(a) kufanya mapitio ya huduma zilizojumuishwa katika kitita hicho;

(b) kufanya mapitio ya bei za huduma za afya katika kitita ili ziendane na bei halisi kwa kipindi husika; au

(c) kufanya mapitio ya viwango vya uchangiaji katika kitita kwa kuzingatia gharama halisi za utoaji wa kitita hicho.

(2) Maboresho ya kitita cha mafao ya huduma muhimu katika kanuni ndogo ya (1) yatazingatia tathmini ya uhai na undelevu wa skimu za bima ya afya.

Uzingatiaji wa taratibu za rufaa

33.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 21 cha Sheria, mwanachama au mnufaika ambaye hatazingatia utaratibu wa rufaa wakati wa kupata huduma

za afya atawajibika kulipia gharama za matibabu katika kituo cha afya alichohudumiwa.

(2) Kituo cha kutolea huduma za Afya, kitatoa huduma zaAfya kwa Mwanachama au mnufaika wa Bima ya Afya kwa kuzingatia utaratibu wa Rufaa

(3) Skimu ya bima ya afya haitawajibika kulipa madai yaliyowasilishwa kwake na kituo cha huduma za afya yanayohusu Mwanachama au mnufaika ambaye hatazingatia masharti ya kanuni ndogo (1) na (2)

Miongozo ya utoaji wa kitita cha mafao ya huduma muhimu

34. kwa kuzingatia kifungu cha 21 cha Sheria, utoaji wa kitita cha mafao ya huduma muhimu kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya Taifa utazingatia miongozo ya Wizara.

*(b) Kitita cha huduma za ziada*

Kitita cha huduma za ziada

35. Kwa madhumuni ya uanzishwaji wa kitita cha huduma za ziada, Mamlaka itaandaa mwongozo wa utoaji wa kitita hicho ambapo, pamoja na mambo mengine, masuala yafuatayo yatazingatiwa-

(a) huduma zitakazojumuishwa katika kitita cha huduma za ziada zitakuwa ni zaidi ya huduma zilizojumuishwa katika kitita cha mafao ya huduma muhimu; na

(b) viwango vya uchangiaji wa kitita cha huduma za ziada vitazingatia tathmini ya uhai na uendelevu wa skimu katika kutoa huduma hizo.

## SEHEMU YA SABA
## UTARATIBU WA MALIPO KWA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Uwasilishaji wa madai

36.-(1) Kituo cha kutolea huduma za afya kitawasilisha katika skimu ya bima ya afya madai ya huduma zilizotolewa kwa mwanachama na mnufaika ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kukamilika kwa huduma kwa mwanachama.

(2) Kituo cha kutolea huduma za afya

kitawasilisha madai kwa kuzingatia miongozo itakayotolewa na skimu za bima ya afya na kuidhinishwa na Mamlaka.

(3) Kituo cha kutolea huduma za afya kitakachowasilisha madai yake nje ya muda uliotajwa katika kanuni ndogo ya (1) kitatakiwa kutoa sababu za msingi kwa skimu ya bima ya afya husika kabla ya madai yake kukubaliwa au kukataliwa:

Isipokuwa kwamba, kituo kitatakiwa kuwasilisha madai hayo ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kuisha muda uliorejewa katika kanuni ndogo ya (1).

Ulipaji wa madai

37.-(1) Skimu ya bima ya afya ndani ya siku tatu tangu tarehe ya kupokea madai ya kituo cha huduma za afya itakitaarifu kituo husika kuhusiana na madai hayo na itapaswa kulipa madai halali ndani ya kipindi kisichozidi siku Sitini tangu tarehe ya kupokea madai.

(2) Bila kujali kanuni ndogo (1), iwapo skimu kwa sababu yoyote ya msingi, itashindwa kulipa madai halali ya kituo cha kutolea huduma za afya ndani ya kipindi kilichorejewa katika kanuni ndogo (1), skimu ya bima ya afya inaweza kuongeza muda wa malipo usiozidi siku kumi na tano:

Isipokuwa kwamba skimu ya bima ya afya itapaswa kutoa taarifa ya kusudio la kuongeza muda wa malipo kwa kituo cha kutolea huduma za afya angalau siku kumi na tano kabla ya muda wa malipo kuisha, na itawasilisha nakala ya taarifa hiyo kwa Mamlaka.

(3) Skimu ya bima ya afya itaweka utaratibu wa malipo kwa vituo vya kutolea huduma za afya utakaoidhinishwa na Mamlaka kwa kuzingatia maslahi ya vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya.

(4) Skimu ya bima ya afya itakayoshindwa kulipa madai kwa kituo ndani ya muda ulioainishwa katika kanuni ndogo ya (1) na (2), itawajibika kulipa madai hayo pamoja na faini ya asilimia tano ya madai yanayopaswa kulipwa kwa kituo cha kutolea huduma za afya.

Uchunguzi na usuluhishi wa madai

38.-(1) Endapo skimu imebaini kuwa kuna dosari kwenye taarifa ya madai na dosari hizo zinaweza kutatulika, skimu itamtaarifu mtoa huduma za afya kuhusu dosari na kuweka utaratibu wa namna ya kutatua dosari hizo ndani ya kipindi kilichorejewa katika kanuni ya 37.

(2) Endapo skimu imebaini uwepo wa madai yenye viashiria vya udanganyifu kutoka kwa mtoa huduma, skimu itaahirisha ulipwaji wa madai hayo na itayashughulikia madai hayo kwa kuzingatia taratibu zifuatazo-

(a) skimu ya bima afya itakitaarifu kituo husika cha kutolea huduma za afya kwa maandishi kuhusu kuahirisha kwa malipo ya madai yenye utata au viashiria vya udanganyifu na sababu za kuahirisha malipo hayo;

(b) skimu ya bima ya afya itafanya uchunguzi wa madai yenye viashiria vya udanganyifu na itaipa kituo cha huduma za afya taarifa ya matokeo ya uchunguzi na nakala ya taarifa hiyo kwa Mamlaka;

(c) endapo kituo cha huduma za afya hakitaridhishwa na taarifa iliyotolewa na skimu ya bima ya afya, kitaijulisha skimu ya bima ya afya ndani ya siku kumi na tano tangu kupokelewa kwa taarifa na kutoa uthibitisho kwa skimu ya bima ya afya juu ya utetezi wake;

(d) skimu ya bima ya afya itapaswa kutoa maamuzi ndani ya siku kumi na tano tangu kupokelewa kwa utetezi wa kituo cha huduma za afya;

(e) endapo kituo cha huduma za afya hakitaridhishwa na maamuzi ya skimu, kituo hicho kitawasilisha malalamiko kwa Mamlaka ndani ya siku saba baada ya kupokea uamuzi wa skimu.

Ushughulikiaji wa malalamiko
Sura 394

39.-(1) Kwa kuzingatia mamlaka iliyonayo chini ya kifungu cha 6 (1) cha Sheria ya Bima, Mamlaka

itapokea na kushughulikia malalamiko yatakayowasilishwa kwake na skimu ya bima ya afya, kituo cha kutolea huduma za afya, mwanachama au mwajiri.

(2) Malalamiko yanayoweza kuwasilishwa na watu waliotajwa katika kifungu kidogo cha (1), yatatokana na-

(a) malalamiko yatokanayo na kanuni ya 38; au

(b) malalamiko mengine yoyote ambayo Mamlaka itaona yanakidhi kwa lengo kuhakikisha uwepo wa ufanisi, usawa, usalama na uendelevu wa bima ya afya nchini.

(3) Mamlaka itatolea maamuzi ya malalamiko yaliyowasilishwa kwake kwa maandishi kwa kuzingatia mwongozo wa kushughulikia malalamiko utakaowekwa na Mamlaka.

(4) Bila kujali masharti ya kanuni hii, Mamlaka inaweza kuwasilisha malalamiko ambayo itaona kuwa yanakidhi kushughulikiwa na Msuluhishi kwa mujibu wa Sheria ya Bima.

Usuluhishi na utatuzi wa Migogoro
Sura ya 394
TS. Na. 411 ya mwaka 2013.

40-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 124(5) cha Sheria ya Bima na kanuni ya 34(4), Msuluhishi atasuluhisha na kutatua migogoro ya bima ya afya kwa kwa mujibu wa Kanuni za Msuluhishi wa Migogoro ya Bima za Mwaka 2013.

(2) Mtu yoyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Msuluhishi, anaweza kuwasilisha malalamiko yake Mahakama Kuu kwa ajili ya rejea kwa mujibu wa Kanuni za Msuluhishi wa Migogoro ya Bima za Mwaka 2013.

Rufaa dhidi ya maamuzi ya Mamlaka

41.-(1) Mtu yoyote ambaye hajaridhishwa na uamuzi wa Mamlaka chini ya Kanuni hizi, anaweza kukata rufaa kwa Baraza la Rufaa la Bima kwa mujibu wa Sheria ya Bima na Kanuni chini ya Sheria hiyo.

(2) Masharti ya kifungu cha 126(7) cha Sheria ya Bima yatatumika endapo mtu hajaridhishwa na uamuzi wa Baraza la Rufaa la Bima.

Sura ya 394

(3) Endapo skimu ya bima ya afya itakiuka

masharti ya kanuni ndogo ya (2), kituo cha huduma za afya kinaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka kwa kuzingatia utaratibu ulioainishwa katika Sheria ya Bima.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI YA JUMLA

Matumizi ya Kanuni za Bima T.S Na. 372 la 2009

42. Masharti ya Kanuni za Bima za Mwaka 2009, pamoja na mabadiliko yanayobidi, yatatumika pamoja na Kanuni hizi.

Utaratibu wa uwekaji wa amana T.S Na. 372 ya mwaka 2009

43. Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 26 cha Sheria, utaratibu wa uwekaji wa amana kwa skimu bima ya afya binafsi utakuwa kama ulivyoainishwa katika Kanuni za Bima za Mwaka 2009.

Utaratibu wa kuhama skimu

44. Endapo mwanachama aliyejiunga katika skimu ya bima ya afya ataamua kuhama katika skimu husika na kuhamia skimu nyingine, atafuata taratibu za usajili kwa mujibu wa kanuni na miongozo ya Mamlaka.

Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya michango

45. Bila kuathiri masharti ya Sheria, mamlaka za serikali za mitaa zinaweza kuratibu ukusanyaji wa michango ya wananchi kwa ajili ya kuwasajili katika skimu ya bima ya afya kwa lengo la kuwawezesha kunufaika na vitita mbalimbali vitolewavyo na skimu za bima ya afya.

Makosa na adhabu dhidi ya skimu za bima ya afya

46. Endapo, kwa maoni ya Mamlaka, skimu ya bima ya afya-

(a) inaendesha shughuli za bima ya afya pasipo kuzingatia misingi ya undeshaji bima inayokubalika;
(b) inaendesha shughuli zake pasipo kujali maslahi ya wanachama na wanufaika;
(c) inaendesha shughuli za bima kwa kutozingatia miongozo inayotolewa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi;
(d) imeshindwa kuwasilisha taarifa zinazohitajika na Mamlaka katika muda uliowekwa;

(e) kwa makusudi, imetoa taarifa za upotoshaji kwa Mamlaka;

(f) imeshidwa kuzingatia vigezo na masharti ya usajili au kushindwa kutii maelekezo yoyote ya awali yaliyotolewa kwake,

Skimu hiyo itakuwa imetenda kosa na itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni hamsini.

Hatua ambazo Mamlaka inaweza kuchukua dhidi ya skimu ya bima ya afya.

47.-(1) Mamlaka, pamoja na hatua nyingine yoyote inayoweza kuchukuliwa, inaweza-

(a) kuiweka skimu ya bima ya afya chini ya uangalizi;

(b) kutoa amri ya katazo ya kusitishwa kwa skimu;

(c) kutoa maelekezo kwa skimu ya bima ya afya;

(d) kuteua msimamizi wa muda kwa lengo la kusimamia uendeshaji wa skimu ya bima ya afya, na itabainisha malipo ya usimamizi ambayo yatapaswa kulipwa na skimu ya bima ya afya;

(e) kuzuia uendeshaji wa skimu ya bima ya afya hadi pale ambapo jambo lililopelekea kuwekewa zuio limetatuliwa;

(f) kusitisha idhini yoyote inayokusudiwa kutolewa na Mamlaka;

(g) kuchukua hatua za kumuondoa au kumsimamisha mtu yeyote katika nafasi ya uongozi wa skimu ya bima ya afya au kumzuia mtu huyo kushiriki katika shughuli za uendeshaji wa skimu ya bima ya afya;

(h) kutoza faini kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi.

(i) kusitisha usajili wa skimu ya bima ya afya; au

(j) kuchukua hatua yoyote nyingine muhimu kwa lengo la kurekebisha jambo lolote linalohitaji kurekebishwa.

(2) Mtu yeyote ambaye hajaridhika na amri au maelekezo ya Mamlaka chini ya kanuni hii, anaweza,

ndani ya siku thelathini, kukata rufaa kwa Baraza la Rufaa la Bima.

Kufuta TS Na 359 ya 2004

48. Kanuni za Mfuko wa Afya ya Jamii za mwaka 2004 zinafutwa.

JEDWALI

FOMU NA. 1

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 3(1))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

FOMU YA MAOMBI YA KUSAJILIWA KWA SKIMU YA BIMA YA AFYA

SEHEMU A: TAARIFA ZA SKIMU YA BIMA YA AFYA

1. Jina la skimu ya bima ya afya.....................................................

   (a) Halmashauri/ Manispaa..................................

   (b) Wilaya………………………………………………

   (c) Mkoa............................................................

   (d) Makao makuu ya skimu ya bima ya afya.........................

   (e) Anuani ya skimu ya bima ya afya............................

   (f) Namba ya simu................................

   (g) Barua pepe....................................................................

   (h) Mwaka wa fedha wa skimu ya bima ya afya………………………………………

2. Mtendaji Mkuu

   (a) Jina.......................................................................

   (b) Anuani..................................................................

   (c) Namba ya simu..................................................

   (d) Barua pepe.........................................................

   (e) Uraia...................................................................

   (f) Elimu..................................................................

SEHEMU B: TAARIFA ZA UMILIKI NA WAMILIKI WA SKIMU YA BIMA YA AFYA

1. Aina ya skimu ya afya (weka alama ya √)

(a) Umma

(b) Binafsi ☐

2. Wamiliki

(a) Taarifa za Kampuni [ ]

i. Jina la Kampuni............................................................

ii. Mahala Ofisi kuu ilipo.....................................................

iii. Kiasi cha mtaji..............................................................

iv. Taarifa za wajumbe wa Bodi ya wakurungezi wa skimu ya bima ya afya……

v. Taarifa za wafanyakazi wa skimu ya bima ya afya………………………………..

vi. Idadi na maeneo ya ofisi za skimu ya bima ya afya ……………………………….

vii. Taarifa za kibenki za skimu ya bima ya afya…………………………………………

viii. Taarifa za mkaguzi wa nje wa skimu ya bima ya afya……………………………

ix. Taarifa za mshauri wa kisheria wa skimu ya bima ya afya……………………….

x. Nakala zilizothibitishwa za vyeti za hisa kwa wanahisa…………………………

xi. Majina ya wanahisa pamoja na hisa wanazomiliki...............................................

(b) Taarifa binafsi [ ]

(i) Jina la Mmiliki...........................................................................

(ii) Anuani........................................................................................

(iii) Namba ya Simu......................................................................

(iv) Uraia..........................................................................................

3. Idadi ya hisa zilizotolewa na Skimu ya Bima ya Afya………………………………………..

4. Idadi na thamani ya hisa za Skimu ya Bima ya Afya zilizolipiwa…………………………

5. Wawekezaji kwenye Skimu ya Bima ya Afya na idadi ya hisa zao…………………………

Tamko la Mwombaji: Maelezo yaliyotolewa hapo juu ni ya kweli kwa kadri ya ufahamu wangu

Tarehe………………………………mwezi…………………………….
mwaka…………….
Jina la mwombaji………………………………………………………saini…………
Wadhifa wake…………………………………………… Mhuri wa Skimu

FOMU NA. 2

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 7(3))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA

FOMU YA MAOMBI YA KUHUISHA USAJILI/CHETI KIPYA

SEHEMU A: TAARIFA ZA SKIMU YA BIMA YA AFYA

1. Jina na mahali ilipo skimu ya bima ya afya

   (i) Jina la skimu ya bima ya afya.....................................................

   (j) Halmashauri/ Manispaa..................................

   (k) Wilaya………………………………………………

   (l) Mkoa............................................................

   (m) Makao makuu ya skimu ya bima ya afya.........................

   (n) Anuani ya skimu ya bima ya afya............................

   (o) Namba ya simu................................

   (p) Barua pepe....................................................................

   (q) Mwaka wa fedha wa skimu ya bima ya afya………………………………………

2. Mtendaji Mkuu

   (g) Jina........................................................................

(h) Anuani...................................................................

(i) Namba ya simu..................................................

(j) Barua pepe.........................................................

(k) Uraia.....................................................................

(l) Elimu....................................................................

SEHEMU B: TAARIFA ZA UMILIKI NA WAMILIKI WA SKIMU YA BIMA YA AFYA

1. Aina ya skimu ya afya (weka alama ya √)

(c) Umma ☐

(d) Binafsi ☐

2. Mmiliki/Wamiliki

(c) Taarifa za Kampuni [ ]

xii. Taarifa za wajumbe wa Bodi ya wakurungezi wa skimu ya bima

xiii. Taarifa za wamiliki ikiwemo uthibitisho wa uraia…………………………………………

xiv. Nakala zilizothibisha za vyeti vya hisa kwa wanahisa……………………………

xv. Uthibitisho wa mtaji wa skimu ya bima ya afya kwa skimu binafsi…....................

xvi. Jina la Mkurugenzi/ Wakurugenzi.............................................................................

xvii. Majina ya wanahisa pamoja na hisa wanazomiliki...............................................

xviii. Taarifa za wafanyakazi wa skimu ya bima ya afya………………………………..

xix. Idadi na maeneo skimu ya bima ya afya yenye ofisi……………………………….

xx. Taarifa za kibenki za skimu ya bima ya afya…………………………………………

xxi. Taarifa za mkaguzi wa nnje wa skimu ya bima ya afya…………………………………….

xxii. Taarifa za mthamini ya skimu ya bima ya afya……………………………………

xxiii. Taarifa za mshauri wa kisheria wa skimu ya bima ya afya……………………….

xxiv. Taarifa za madai ya skimu ambayo hayajalipwa mpaka Tarehe ya kuhuhisha usajili …

xxv. Taarifa ya kutokuwa na pingamizi kutoka FIU kwa mtu aliyeteuliwa kuwasilisha taarifa FIU…..

(d) Taarifa binafsi [ ]

(v) Jina la Mmiliki..........................................................................

(vi) Anuani......................................................................................

(vii) Namba ya Simu......................................................................

(viii) Uraia..................................................................................

3. Idadi ya hisa zilizotolewa na Skimu ya Bima ya Afya………………………………………..

4. Idadi na thamani ya hisa za Skimu ya Bima ya Afya zilizolipiwa…………………………

5. Wawekezaji kwenye Skimu ya Bima ya Afya na idadi ya hisa zao…………………………

*(Zingatia:Taarifa hizi zitawasilishwa endapo kuna mabadiliko yaliyojitokeza)*

Tamko la Mwombaji: Maelezo yaliyotolewa hapo juu ni ya kweli kwa kadri ya ufahamu wangu

Tarehe………………………………mwezi…………………………….
mwaka…………….
Jina la mwombaji………………………………………………………saini…………
Wadhifa wake…………………………………………… Mhuri wa Skimu

FOMU NA. 3

(*Imetengenezwa chini ya kanuni ya 12(1))*

REJESTA YA SKIMU ZA BIMA YA AFYA

| NA | Jina la Skimu na | Namba ya Simu na | Namba na tarehe ya | Idadi ya wanacham | Taarifa za | Taarifa za vituo | Taarifa nyinginez |
|---|---|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Anuani | barua pepe | usajili | a na wanufaika waliyosaji liwa | waajiri walioingi a mkataba na skimu | vilivyoin gia mkataba na skimu | o |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

Dodoma,
11 septemba, 2024

JENISTA J. MHAGAMA
*Waziri wa Afya*